# MAAKIZO YA KISWAHILI KIDATO CHA TATU

**Riwaya: Nguu za jadi.**

a) Changanua mbinu za kimtindo katika kifungu hiki. ( alama 5)

“Ama kweli,moto ule umenitia taflisi.Nitaishia kula mwande na wanangu.Huko ndiko kufa kingoto,”Mangwasha alijisemea kwa huzuni,lakini akajipa moyo.Miaka huweza kutia ngozi ya mwili makunyanzi.Mangwasha alikuwa na Imani ya kuishi.Imani hiyo uvumilivu na tumaini.Alivifungafunga vile vitu,akawatazama tena wanawe waliolala sakafuni kwenye maabadi yale ya Mungu.Alikumbuka usiku huo alipoingia humo na wanawe kupitia kwa dirisha lililokuwa wazi.Hata alipofaulu,bado alihisi wale watu wanamfuata humo.

**Tashbihi: kufa kikondoo.**

**Nahau: nitaishia kula mwande.**

**Uzungumzi nafsia: Mangwasha alijisemea kwa huzuni.**

**Taswira oni: akawatazama tena wanawe.**

**Mbinu rejeshi: alikumbuka usiku huo alipoingia humo na wanawe.**

b) Eleza kilichokuwa kimesababisha matukio haya. ( alama 4)

**Mangwasha na waketwa wengine walikuwa wamefurushwa kutoka eneo la Matango na nyumba zao kuteketezwa.**

**Mangwasha alitorokea kanisani pamoja na wanawe .Uongozi wa Matuo ulikuwa unawataka waketwa kurudishwa kwao Ndengoni.**

c) Eleza umuhimu wa mandhari ya sura ya pili katika riwaya ya Nguu za jadi. (alama 5)

**Mandhari haya yanakuza maudhui ya ndoa na changamoto zake.**

**Mandhari haya yanakuza sifa za wahusika mbalimbali kama Mrima ni mkengeushi au mwepesi wa kushawishika.**

**Mandhari haya yanaendeleza ploti kwani tunafahamishwa mengi kuhusu utawala wa Mtemi Lesulia.**

**Mandhari haya yanaendeleza maudhui ya ufisadi.**

**Mandhari haya yanaendeleza maudhui ya uwajibikaji.**

**Mandhari haya yanakuza mitindo mbalimbali ya lugha kama vile uhuishi,taswira.**

**Mandhari haya yanakuza migogoro.mfano kati ya Man**gwasha na Chifu Mshabaha.

**(Mwanafunzi adokeze hoja zingine zozote.)**

d) “Alifunzwa kutotumia sifa zake za kike alizokirimiwa na muumba kustarehesha wanaume ili kujinufaisha.”

i. Eleza muktadha wa dondoo hili. ( alama 4

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

Teacher.co.ke

**Haya ni maneno ya mwandishi akimrejelea Mangwasha.Mangwasha alikuwa kanisani na wanawe walipokwenda kujinusuru kutoka kwa hasidi zao.Hivyo Mangwasha hakutegemea msaada wowote kwa mtu ili kujinufaisha.**

ii. Kwa kutolea mifano,onyesha jinsi baadhi ya wahusika wa kike wanavyotumia sifa za kike kujinufaisha kutokana na wanaume. ( alama 2)

**Sihaba . Anajihusisha kimapenzi na Sagilu ili anufaike maishani.**

**Cheiya. Anawategemea wanaume kwa msaada kwa matatizo yake ya pesa na hivyo pia anahusiana na Sagilu.**

**Tamthiliya: Bembea ya maisha**

a) Changanua mtindo katika kifungu hiki. ( alama 5)

“Bunju ni mmoja wenu.Nyote ni wanangu.Hayo ni maneno ya mama.Wakati huo sikuona.Sasa ninaona.Wanasema mwenye macho haambiwi tazama.Kweli iliyoje!Japo hutokea wakati tukalalamika.Ninafikiri Bunju ni zawadi nzuri kwetu.Leo tungekuwa wapi bila Bunju?Maji yangezidi unga,usingepikika,usingelika.Hebu fikiri!Umepata ajali mbaya.Inakuacha mahututi.Anapita mtu katika gari lake.Kwa Imani anaguswa.Anakufanyia mpango wa flying doctors..

**Mbinu rejeshi: Neema anakumbuka maneno ya mamake kuhusu umuhimu wa Bunju katika maisha yao.**

**Methali: mwenye macho haambiwi tazama.**

**Nidaa: kweli iliyoje!**

**Msemo: Maji yangezidi unga.**

**Kuchanganya ndimi: Anakufanyia mpango wa flying doctors.**

**Uzungumzi nafsia:wakati huo sikuona sasa ninaona.**

b) Msemaji wa maneno haya ni kielelezo cha uwajibikaji.Fafanua. (alama 8)

**Neema anawajengea wazazi wake nyumba.**

**Neema anafadhili masomo ya wanuna zake.**

**Neema anawaajiria wazazi wake wafanyakazi.**

**Neema pia anampeleka mamake shuleni.**

**Neema anampeleka lemi mwanawe out.**

**(Mwanafunzi aongezee hoja zingine zozote sahihi.)**

c) Tambua toni katika kifungu hiki.( alama 2)
**Toni ya huzuni.hebu fikiri! Umepata ajali mbaya.**

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

## Ushairi

**Soma shairi lifuatalo Kisha ujibu maswali.**

Watafuta riziki, watatokwa jasho vijijini
Wakulima shakiki, wakuza chai na mbuni
Vyakula washakiki, visipungue vinyuani.

Watafuta riziki, wahangaikao mijini
Kutwa kile na hiki, kama watanga na mipini
Japo hawasikii, hawakosi kujiamini.

Watafuta riziki, wazalendo wa nchi hii
Kamwe hawajidhiki, tama za moyo kutii
Bali huafiki, kupingana na ulaghai

Watafuta riziki, pato ambalo la halali
Ndoto haizimiki, ya kesho kuwa njema Hali
Wiki baada ya wiki, la haramu jasho hawali.

**Maswali**

a) Taja anwani inayoafiki shairi hili. (alama 2)
**Watafuta riziki.**

b) Ainisha shairi hili kwa kuzingatia vigezo vifuatavyo.(alama3)
  i. Idadi ya mishororo. **Tathlitha**
  ii. Mpangilio wa vina. **Ukara**
  iii. Mpangilio wa maneno. **Kikwamba**

c) Eleza kwa kutia mifano,mbinu tatu ambazo mshairi ametumia kutosheleza mahitaji ya kiarudhi. (alama 3)
**Utohozi: wiki**
**Mazda: vinyuaji badala ya vinywaji**
**Inksari:tama badala ya tamaa.**
**Kuboronga sarufi: la haramu jasho hawali badala ya hawali jasho la haramu.**

d) Bainisha tamathali mbili za usemi katika shairi hili. ( alama 3)
**Takriri: watafuta riziki**
**Taswira: Japo hawasikii**
**Uhuishi:tama za moyo kutii**
**Tashbihi: kutwa kile na hiki kama watanga na mipini.**
**Taashira:watatokwa jasho vijijini „ishara ya bidii.**

e) Eleza muundo wa shairi hili. ( alama 4)

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes

**Shairi hili lina beti nne.**
**Kila mshororo una vipande viwili.**
**Halina kibwagizo.**
**Kila mshororo una mizani kumi na sita.**
**Kila ubeti una mishororo mitatu.**

Download this and other FREE materials from https://teacher.co.ke/notes

Download this and other FREE revision materials from https://teacher.co.ke/notes